



# NISHATI

HABARI ZA  
NISHATI

# News **Bulletin**

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz) [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara ya Nishati) [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania) [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017) [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara ya Nishati)

Toleo Namba 16

Julai 1-31, 2020

## SERIKALI YAANZA RASMI BIASHARA YA KUUZA MAFUTA NCHINI

»»» Dkt. Kalemami afungua Kituo cha  
kwanza Mara, TPDC kujenga vituo 100



»»» UK.  
2

Mwonekano wa Kituo cha kuuza mafuta ya petroli na dizeli cha serikali (TANOIL) kitakachosimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kupitia Kampuni ya Mafuta ya TANOIL, kilichofunguliwa na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami, (kulia) Juni 06, 2020 wilayani Musoma mkoani Mara.

## WAZIRI KALEMANI ATOA ONYO KWA WANAOFICHA MAFUTA



UK.  
7



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au  
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma



Mwonekano wa Kituo cha kuuza mafuta ya petroli na dizeli cha serikali (TANOIL) kitakachosimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kupitia Kampuni ya Mafuta ya TANOIL, kilichofunguliwa na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami, Juni 06, 2020 wilayani Musoma mkoani Mara.

# Serikali yaanza rasmi biashara ya kuuza mafuta nchini

**Zuena Msuya - Mara**

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami amezindua rasmi biashara ya kuuza na kusambaza mafuta kwa Serikali nchini kwa kufungua kituo cha kwanza cha kuuza mafuta ya Petroli na Dizeli kitakachosimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kupitia Kampuni yake Tazungu ya Mafuta (TANOIL).

Dkt. Kalemami alisema kuwa kuzinduliwa na kufunguliwa kwa biashara hiyo ni kutimiza azma na nia njema ya Serikali ya kuboresha shirika lake la TPDC, kuwapatia

na kuwasogezea karibu wananchi wake huduma ya kupata mafuta yenye viwango vya ubora unaotakiwa, bei nafuu, na yatakayopatikana kwa wingi muda wote.

Alifanya uzinduzi huo pamoja na kufungua kituo hicho wilayani Musoma, mkoani Mara Juni 6, 2020, wakati wa ziara yake ya kikazi katika Mkoa huo, akiwa ameambatana na Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu, Katibu Mkuu Mhandisi Zena Said pamoja na viongozi wengine waandamizi wa wizara na taasisi zilizo chini yake.

Alisema, baada ya kuanza rasmi kwa biashara hiyo, TPDC kupitia TANOIL itashirikiana na halmashauri zote nchini

kuhakikisha inafanikisha azma ya Serikali ya kufungua na kuweka vituo vya kuuza na kusambaza mafuta katika kila halmashauri nchini pamoja na miundombinu ya kuhifadhi na kusafirisha mafuta.

“Tumeshaanza biashara ya kuwauzia wananchi wetu mafuta, sitegemei kusikia mafuta yanauzwa kwa bei ghali katika vituo vya serikali. TPDC na TANOIL mnielewe vizuri hapa! Lengo letu sisi serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata bidhaa bora za mafuta kwa kiwango kinachotakiwa, kwa bei nafuu na kwa wingi, wakati wote,” alisema Dkt. Kalemami.

Aidha, alibainisha

kuwa TPDC na TANOIL watashiriki katika biashara ya uagizaji na usambazaji mafuta kama zinavyofanya kampuni nyingine za mafuta nchini ili kuongeza ushindani na kutanua wigo wa kampuni za kizalendo kushiriki katika biashara ya mafuta, ambayo kwa sasa inafanywa na kampuni kutoka nje ya nchi tu.

Alisema kuwa, Serikali kupitia TPDC itajenga vituo 100 kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, ambapo tayari baadhi ya halmashauri zimeanza kutenga maeneo yatakayojengwa vituo hivyo. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa nusu ya



# BODI YA UHARIRI

**Mhariri**

**Veronica Simba**  
(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini)

**Waandishi**

**Veronica Simba**  
**Teresia Mhagama**  
**Zuena Msuya**  
**Hafsa Omar**

**Msanifu Kurasa**

**Lucas Gordon**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018  
Nukushi: +255-26-2320148  
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano Mtumba Dodoma, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

- [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)
- [Wizara ya Nishati](#)
- [@Nishati2017](#)
- [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)
- [Wizara ya Nishati](#)

## WAFANYABIASHARA WA MAFUTA SOMENI ALAMA ZA NYAKATI

**T**angu Serikali itangaze bei elekezi mpya ya mafuta, ambayo imeshuka kulinganisha na iliyokuwepo awali, kumekuwepo na taarifa za baadhi ya wafanyabiashara wa mafuta, kutouza bidhaa hiyo, ikidaiwa wanasubiri bei ipande ndiyo wauze.

Hali hiyo siyo tu imekuwa ikisababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi, bali pia imekuwa ikiikosesha mapato Serikali. Aidha, ni kinyume cha sheria za nchi.

Juni 15 mwaka huu, Waziri mwenye dhamana na sekta ya nishati, Dkt Medard Kalemani aliamua kuzungumza na Waandishi wa Habari jijini Dodoma, kwa lengo la kuwaonya wafanyabiashara wenye tabia hiyo kuacha mara moja.

Waziri aliwataka wafanyabiashara hao kutambua kuwa wanatoa huduma kwa wananchi, hivyo wanawajibika kisheria kuenenda kadri ya matakwa ya leseni zao.

Siyo hivyo tu, bali pia Waziri aliiagiza Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa kushirikiana na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), kufuatilia suala hilo ili kuwabaini wale wanaoficha mafuta na kuwawajibisha.

Kufuatia agizo hilo la Waziri, tumeshuhudia kupitia vyombo vya


habari, baadhi ya wamiliki wa vituo vya mafuta nchini wakikamatwa na Polisi kwa tuhuma hizo. Tunazipongeza Mamlaka husika kwa kuamua kulivalia njuga suala hilo ili kukomesha kabisa tabia hiyo isiyo na uzalendo.

Tunaamini kwa hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali dhidi ya wanaohusika na vitendo vya kuficha mafuta, kutakomesha vitendo hivyo na kuwaondolea adha wanayoipata wananchi kutokana na kuadimika kwa bidhaa hiyo.

Niwakumbushe tu wafanyabiashara wa mafuta wanaoficha mafuta na kuwatesa wananchi, wajifunze kusoma alama za nyakati. Serikali hii ni ya kazi na iko kazini kwelikweli. Hakuna mzaha. Kitendo cha kuficha mafuta ni kui-“beep” Serikali na bila shaka watapata wanachokitafuta.

Nimalize kwa kuwashauri wafanyabiashara hao kuchagua kusuka au kunyoa. Kama wanapenda kuendelea na biashara yao basi na waifanye kwa uaminifu na kwa kufuata sheria. Na kama siyo hivyo, waachane na biashara hiyo, wawapishe wale wanaoweza kufuata sheria wafanye kazi hiyo. Hapa ni kazi tu.

## Katunika Ki-nishati



Copyright  
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI  
WIZARA YA NISHATI (2020)

# Serikali yaanza rasmi biashara ya kuuza mafuta nchini

INATOKA UK.

2

mafuta yote yanayoingizwa nchini yanasimamiwa TPDC.

“Watanzania tutembea kifua mbele na kujivunia vilivyo vya kwetu. Uzinduzi wa biashara hii ya mafuta hapa Musoma leo unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, ya Uongozi wa Rais Dkt. John Magufuli, ni kutambua juhudi na mchango mkubwa wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kuimarisha sekta ya Umma ya kukuza uchumi.”

Alisema Watanzania hawana budi kutambua mchango wa Mwalimu kuanzisha TPDC mwaka 1969 pamoja na kiwanda cha kusafisha mafuta cha TIPER mwaka huohuo, ambapo TPDC ilimiliki kiwanda hicho kwa asilimia 50%. “Mwalimu aliona na kuwaza mbali sana, yote ikiwa ni katika dhana ya

kujitegemea kiuchumi,” alisisitiza Dkt. Kalemami.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio alisema kuwa katika kutekeleza azma hiyo ya serikali, kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021, TPDC imetenga fedha za kutosha kwa ajili ya mtaji wa kugharamia shughuli za uagizaji, usambazaji na usimamizi wa mauzo ya mafuta nchini kote.

Alisema kwamba TANOIL imejipanga kuhakikisha kunakuwa na usalama wa usambazaji mafuta nchini, kunapatikana takwimu sahihi za mafuta, bei na viwango stahiki vya ubora pamoja na uelewa mzuri na mpana wa biashara ya mafuta nchini.

“Nina furaha sana leo TPDC inaandika historia mpya na kubwa sana katika nchi yetu. Tunaungana na wakazi wa Mkoa wa Mara, kwa niaba ya Watanzania wote kuonesha furaha yetu

katika kuandika historia hii mpya ya kwamba shirika letu linarudi kwa kishindo katika biashara ya kuuza na kusambaza mafuta na bidhaa zake kwa maslahi yetu sote na taifa kwa ujumla.

Alieleza zaidi kuwa mwaka 2000, Serikali ilifanya maamuzi ya kuendesha biashara ya mafuta nchini kwa mfumo wa soko huria, hivyo TPDC ikaunda kampuni tanzu ya COPEC kuweza kuingia katika mfumo huo na kushiriki katika soko la ushindani katika biashara hiyo.

TPDC ilinunua na kujenga vituo mbali mbali nchini vikiwemo Segera na Muheza Mkoani Tanga, Makuyuni na Makumira Mkoani Arusha, Singida, Geita pamoja na Mara ambapo vilinunuliwa vituo viwili tu cha Musoma na Tarime. Alisema vituo vyote hivyo vinamilikiwa na TPDC kwa asilimia 100.

Alizidi kufafanua kuwa

TPDC ilishiriki katika biashara hiyo kupitia katika vituo hivyo lakini kukosekana kwa sheria madhubuti ya Mafuta/Petroli, kulififisha ushiriki wake katika soko lenye ushindani mkubwa.

Alisema, baada ya kufanyika michakato na mapitio ya rejea na maboresho mbalimbali ya shirika hilo kumewezesha uwepo wa sheria madhubuti, pamoja na usimamizi wa kanuni mbalimbali, ambazo sasa zinaiwezesha TPDC kuingia katika soko kwa ufanisi zaidi.

Mataragio alieleza kuwa katika mwaka huu wa fedha, TPDC itakamilisha ujenzi wa vituo viwili katika Mkoa wa Singida na Mkoa wa Geita. Aidha, alisema kuwa shirika hilo linaendelea na mkakati wa kutwaa ardhi katika mikoa

INAENDELEA UK.

5



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemami (wa tatu kushoto), akikata utepe kuashiria ufunguzi wa kituo cha kuuza mafuta ya dizeli na petroli cha serikali (TANOIL) Juni 06, 2020 wilayani Musoma mkoani Mara. Pamoja naye pichani kutoka kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu, Mkuu wa Mkoa wa Mara Adam Malima, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Dkt. James Mataragio na viongozi waandamizi wa Wizara na Taasisi zake.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemami akikata kifungio katika gari iliyobeba mafuta, ili kufungua koki kuruhusu mafuta kuingia katika matanki ya kuhifadhi mafuta ya kituo cha kuuza mafuta ya petroli na dizeli cha TANOIL. Waziri alizindua rasmi biashara ya mafuta katika kituo hicho cha Serikali Juni 06, 2020 wilayani Musoma, mkoani Mara.

# Serikali yaanza rasmi biashara ya kuuza mafuta nchini

INATOKA UK.

4

ya Dar es salaam, Tanga, Dodoma na Morogoro kwa ajili ya kuendesha biashara hiyo.

“Natumia fursa hii kwa niaba ya TPDC kutoa shukrani zetu za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Nishati unayoongoza wewe Dkt. Kalemmani kwa umahiri, kwa maelekezo na rasilimali fedha zinazoiwezesha TPDC sasa kuingia katika biashara hii.”

Pia, alitoa shukrani kwa uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Mara kwa ushirikiano waliotoa katika kipindi chote tangu enzi za COPEC hadi sasa TANOIL na kufungua ukurasa mpya

wa mafanikio ya uzinduzi wa biashara ya mafuta.

Naye Mkuu wa Mkoa huo, Adam Malima, aliwaasa wakazi, wafanyabiashara na watumiaji wa mafuta ya Petroli na Dizeli kuunga mkono juhudi za serikali za kuanzisha bishara ya mafuta kwa kununua mafuta katika vituo vya serikali.

Sambamba na hilo, alisema kuwa kutokana na mikakati iliyowekwa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati kufikisha huduma ya mafuta hayo karibu na wananchi, kutawaweka katika mazingira salama na rafiki watumiaji wa mafuta hayo hasa waendesha bodaboda na wafanyabiashara wadogo.

“Wafanyabiashara wadogo wanaowauzia



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemmani (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi waandamizi wa Wizara na Taasisi zake pamoja na viongozi wa Serikali ya Mkoa wa Mara, baada ya ufunguzi wa kituo cha kuuza mafuta ya dizeli na petroli cha serikali (TANOIL) Juni 06, 2020 wilayani Musoma, mkoani Mara.

waendesha bodaboda na vyombo vingine vidogo vinavyotumia mafuta hayo, wamekuwa wakihifadhi bidhaa hiyo katika hatari kubwa ya kupoteza maisha na mali zao, wanatumia vifungashio duni kama galoni na chupa za maji. Hii itaondoa kabisa hatari iliyopo katika jamii yetu hasa vijijini,” alisema Malima.

Historia inatuonesha kwamba katika miaka ya 80 hadi kufikia Mwaka 2000, TPDC licha ya biashara yake kuu ya utafutaji, uchimbaji, uendelezaji na usambazaji wa gesi

asilia, ilikuwa muagizaji, muingizaji na msambazaji mkuu wa mafuta yote yaliyotumika nchini.

TPDC iliingiza mafuta ghafi nchini na kuyasafisha, na pia uingizaji wa ziada ya mafuta yaliyosafishwa na kutosheleza mahitaji ya mafuta nchini.

Pia TPDC ilibeba jukumu hilo kwa ufanisi na uzalendo wa hali ya juu, ikiwemo kuwa msambazaji pekee aliyesambaza mafuta mstari wa mbele wakati wa vita vya Kagera kati ya Mwaka 1977/78 baada ya kampuni binafsi kugoma kupeleka mafuta Kagera.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani, akizungumza na wakazi wa Mkoa wa Mara wakati akifungua rasmi kituo cha kuuza mafuta ya dizeli na petroli cha Serikali (TANOIL) Juni 06, 2020, wilayani Musoma, mkoani Mara.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio akizungumza na wakazi wa Mkoa wa Mara wakati wa ufunguzi wa kituo cha kuuza mafuta ya dizeli na petroli cha Serikali (TANOIL). Kituo hicho kilifunguliwa rasmi na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani, Juni 6, 2020, wilayani Musoma mkoani humo.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami (kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima wakijadiliana jambo wakati wa ufunguzi wa kituo cha kuuza mafuta ya dizeli na petroli cha Serikali (TANOIL). Dkt. Kalemami alifungua kituo hicho Juni 06, 2020, wilayani Musoma, Mkoa wa Mara.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza na wakazi wa Mkoa wa Mara wakati wa ufunguzi wa kituo cha kuuza mafuta ya dizeli na petroli cha Serikali (TANOIL). Kituo hicho kilifunguliwa rasmi na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami, Juni 6, 2020, wilayani Musoma mkoani humo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said akizungumza na wakazi wa Mkoa wa Mara wakati wa ufunguzi wa kituo cha kuuza mafuta ya dizeli na petroli cha Serikali (TANOIL). Kituo hicho kilifunguliwa rasmi na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami, Juni 6, 2020, wilayani Musoma mkoani humo.

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami (kulia) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Mafuta ya TANOIL, ambayo ni kampuni tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mhandisi Kapuulya Musomba, wakijadiliana jambo wakati wa ufunguzi wa kituo cha kuuza mafuta ya dizeli na petroli cha Serikali (TANOIL). Dkt. Kalemami alifungua kituo hicho Juni 06, 2020, wilayani Musoma mkoani Mara.



## SERIKALI YATOA ONYO KWA WANAOFICHA MAFUTA

**Veronica Simba na  
Zuena Msuya – Dodoma**

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amesema Serikali itawachukulia hatua kali wafanyabiashara wa mafuta nchini, wanaoficha bidhaa hiyo ili wayauze kwa bei kubwa hapo baadaye, hali inayosababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji wake.

Alitoa kauli hiyo Juni 15, 2020 jijini Dodoma, katika mkutano wake na waandishi wa habari.

Alisema, kumekuwepo na taarifa za baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wa mafuta kutotaka kuuza bidhaa hiyo kwa sababu bei elekezi ziko chini kwa sasa, wakisubiri bei zipande ili wapandishe bei na kuwaumiza Watanzania. Waziri amesisitiza kuwa kamwe Serikali haitaruhusu jambo hilo.

“Natoa rai kwa wafanyabiashara wa mafuta ya aina zote nchini ikiwemo petroli, dizeli na mafuta ya taa waache kuficha mafuta. Yeyote tutakayemkamata akificha mafuta, tutamchukulia hatua kali sana za kisheria na kiutawala,” alisisitiza.

Katika kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa, Waziri alitoa maelekezo kwa Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) pamoja na Wakala wa Uagizaji Mafuta Kwa Pamoja (PBPA), kuendesha msako kwa wote wanaoficha mafuta ili kuwabaini na kuwachukulia hatua chini ya Sheria ya EWURA.

Akifafanua, alisema Sheria ya EWURA imeainisha adhabu za aina



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na Waandishi wa Habari (hawapo pichani) katika ofisi za Wizara Dodoma, akiwaonya baadhi ya wafanyabiashara wa mafuta ya Petroli, Dizeli na Taa, kuacha tabia ya kuficha bidhaa hiyo. Mkutano huo ulifanyika Juni 15, 2020.

mbili kwa watakaobainika kutenda kosa la aina hiyo, akizitaja kuwa faini isiyopungua shilingi milioni 100 pamoja na muhusika kufungiwa biashara yake.

Alitoa tahadhari kwa wafanyabiashara wa mafuta akiwataka wakumbuke kuwa wanatoa huduma kwa wananchi, hivyo ni lazima wazingatie masharti ya leseni zao.

“Nawataka watoe huduma na kufanya biashara pasipo kuathiri mapato ya Serikali wala kuathiri upatikanaji wa

mafuta kwa walaji.”

Katika hatua nyingine, Waziri aliwataka wafanyabiashara hao kuendelea kuleta mafuta huku akiwataka wananchi kuondoa shaka juu ya kiwango cha akiba ya bidhaa hiyo kilichopo nchini, akisema ni toshelevu.

“Tunayo akiba kubwa sana ya matanki yetu hapa nchini inayoweza kufikia lita bilioni 1.2 na tunaweza kuitumia kwa muda wa miezi mitatu ijayo. Mahitaji yetu kwa muda huohuo ni lita milioni 750 tu, kwahiyoy uwezo wetu

wa kuhifadhi mafuta ni mkubwa kuliko mahitaji yetu,” alifafanua.

Akizungumzia mchango wa Bandari zilizopo nchini katika suala hilo, Dkt Kalemani alisema kuwa lengo la kuanzishwa kwa Bandari hizo zilizopo Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ni pamoja na kusogeza huduma kwa wananchi ili kila kona ya nchi iweze kupata huduma husika kwa urahisi, kwa haraka na gharama nafuu.

## SERIKALI YATOA ONYO KWA WANAOFICHA MAFUTA

INATOKA UK.

7

Alitoka wito kwa wafanyabiashara na wenye matumizi ya bandari, kuhakikisha wanatumia utaratibu wa bei linganifu ili wananchi pia wafaidi uwepo wa bandari hizo nchini.

Alisema rai hiyo inakwenda sambamba na agizo kwa wafanyabiashara wote wa mafuta, kuhakikisha bei ya mafuta kwa watumiaji inaendelea kushuka kwani katika Soko la Dunia, bei ingali inashuka.

“EWURA lazima mzingatie hili. Akipatikana mfanyabiashara wa kituo cha mafuta anauza bei tofauti na bei elekezi ya Serikali, huyo akamatwe mara moja. Lazima tuhakikishe kushuka kwa bei kunawanufaisha Watanzania.”



Waandishi wa Habari kutoka vyombo mbalimbali nchini, wakiwa katika kikao cha Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (Meza Kuu-katikati), ambapo alikuwa akitoa maelekezo kwa baadhi ya wafanyabiashara wa mafuta ya Petroli, Dizeli na Taa, kuacha tabia ya kuficha bidhaa hiyo. Kikao Mkutano huo ulifanyika katika Ofisi za Wizara, Dodoma, Juni 15, 2020.

Aidha, Waziri alizungumzia suala la upelekaji nishati vijijini, akisisitiza kwamba kwa

upande wa umeme, Serikali imepata mafanikio makubwa kiasi cha kushika nafasi ya kwanza

Afrika kwa usambazaji umeme vijijini.

Hata hivyo, alitanabaisha kuwa, nishati siyo umeme peke yake, hivyo akatoa msukumo kwa Mamlaka zinazohusika kuhakikisha mafuta na gesi pia zinafikishwa kwa wananchi walioko vijijini.

Alisema kwa upande wa gesi, tayari zoezi la kupeleka vijijini limeanza kwa kufikisha nishati hiyo Lindi vijijini na kwa upande wa mafuta, alisema EWURA wanakamilisha taratibu za kuanzisha Mradi wa Kielelezo unaolenga kuanzisha vituo vya mafuta vya gharama nafuu vijijini.

Aliitaka EWURA kuhakikisha ndani ya miezi sita Mradi huo uwe umeanza kutekelezwa kwa kuanza kuruhusu ufunguzi wa vituo vidogo vidogo na huduma tembezi za kuuza mafuta vijijini ili wananchi wa maeneo hayo wanufaike.

Akifafanua zaidi, Waziri alisema endapo Mradi huo wa Kielelezo utaonesha mafanikio, Serikali itaanzisha miradi ya aina hiyo katika maeneo mengi zaidi lakini ikijikita katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi kutokana na miundombinu isiyo rafiki, visiwani na katika maeneo tengefu.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja, Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi pamoja na viongozi waandamizi kutoka EWURA.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati), akizungumza na Waandishi wa Habari (hawapo pichani) katika ofisi za Wizara Dodoma, akiwaonya baadhi ya wafanyabiashara wa mafuta ya Petroli, Dizeli na Taa, kuacha tabia ya kuficha bidhaa hiyo. Mkutano huo ulifanyika Juni 15, 2020. Kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na kushoto ni Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Leonard Masanja.



# WATANZANIA WAANZA KUNUFAIKA NA MRADI WA JNHPP

**Veronica Simba – Dodoma**

**K**atibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said amesema kuwa mradi mkubwa wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) umeanza kuwanufaisha Watanzania hata kabla ya kukamilika.

Aliyasema hayo Juni 22, 2020 alipofanya mahojiano na mwandishi wa habari hii kuhusu ziara ya Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali iliyofanyika Juni 20, mwaka huu kukagua maendeleo ya Mradi huo ulioko Rufiji, mkoani Pwani.

Mhandisi Said aliyataja mafanikio hayo kuwa ni ajira kwa Watanzania pamoja na matumizi ya malighafi za ndani ya nchi, katika ujenzi wa Mradi husika.

Alisema kuwa Ujumbe



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said.*

wa Makatibu Wakuu hao walioshiriki ziara husika, ulifurahishwa kujionea kwamba asilimia kubwa ya wafanyakazi walioko katika Mradi huo ni Watanzania.

Aidha, walifurahishwa kuona kuwa malighafi zinazotumika zinatoka Tanzania.

“Nchi yetu imeanza kunufaika kabla Mradi huu haujakamilika, hususan katika upande wa wafanyakazi na malighafi. Kwahiyo, uchumi umeanza kukua katika hatua hii ya utekelezaji wa Mradi,” alisema.

Aliongeza kuwa, Mradi utakapokamilika, Serikali inatarajia kupata umeme wa uhakika na wenye gharama nafuu ambao utasaidia zaidi katika kuendesha viwanda vilivyopo pamoja na kuhamasisha vingine vije kuwekeza.

Katibu Mkuu huyo mwenye dhamana na Mradi wa JNHPP, alimshukuru Rais John Magufuli kutenga fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati, ukiwemo huo

wa Julius Nyerere, akisema kuwa ni miradi ambayo itaipeleka nchi yetu mbele.

Akizungumzia manufaa zaidi yatakapopatikana baada ya ujenzi wa Bwawa katika Mradi husika kukamilika; alisema nchi itaingia kwenye ramani siyo tu ya Afrika bali pia ya dunia ikiwa ni miingoni mwa nchi zenye mabwawa makubwa ya kuzalisha umeme wa uhakika.

Awali, akizungumza baada ya ziara hiyo ya Makatibu Wakuu, Kiongozi wa Msafara, Prof. Sifuni Mchome, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, alipongeza hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi husika, akisema wameridhishwa na kufurahishwa na maendeleo yake.

“Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu John Pombe Magufuli kwa maono haya makubwa ambayo tunaamini yatakapokamilika, Taifa litakuwa limefunguka na kazi mbalimbali zitakuwa zinaendelea kufanyika katika kujenga uchumi wetu, ili kufikia azma yetu ya uchumi wa kati ifikapo 2025.”

Prof. Mchome alitumia fursa hiyo kuwahakikishia Watanzania kuwa Mradi uko katika hatua nzuri na kwamba utatekelezwa kulingana na ratiba yake, hatimaye kupata umeme ambao Taifa linautegemea.

Ziara ya Makatibu Wakuu hao katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, ni mwendelezo wa ziara za viongozi mbalimbali wa Serikali zinazolenga kuhakikisha Mradi huo unatekelezwa kikamilifu na kwa wakati, kama Serikali ilivyoahidi.



*Kazi ya ujenzi katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha megawati 2,115 ikiendelea.*

# WAZIRI KALEMANI AKAGUA UMEME NYUMBA KWA NYUMBA



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kulia) akiwasili katika kijiji cha Usagara, Wilaya ya Misungwi, Mkoa wa Mwanza, akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme vijijini, Juni 26, 2020.

## Hafsa Omar - Mwanza

**W**aziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, amefanya ziara nyumba kwa nyumba katika vijiji vya Usagara na Isamilo wilayani Misungwi, Mkoa wa Mwanza, Juni 26 mwaka huu, akikagua kazi ya usambazaji umeme.

Akizungumza na wananchi wa kijiji cha Isamilo, Waziri aliwaeleza kuwa lengo lake ni kufahamu idadi ya nyumba ambazo hazijaunganishiwa umeme na kujua sababu zilizofanya nyumba hizo zisiunganishwe ili kutafutia ufumbuzi suala hilo.

“Ndugu zangu wananchi, nimekuwa nikipita kwenye barabara

hii mara kwa mara lakini kila nikitupa jicho mkono wa kushoto naona nyumba

zenu zote hazina umeme jambo ambalo hatuwezi kulikubali,” alisema.

INAENDELEA UK.

11



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (wa kwanza-kulia) akizungumza na mmoja wa wakazi wa kijiji cha Isamilo, wilayani Misungwi, Mkoa wa Mwanza, Restuta Wilbard, alipokwenda kukagua nyumba yake ili iunganishwe umeme, akiwa katika ziara ya kazi, Juni 26, 2020

# WAZIRI KALEMANI AKAGUA UMEME NYUMBA KWA NYUMBA

INATOKA UK.

10

Akieleza zaidi, alisema kuwa mwanzoni mwa mwaka huu (2020), alitoa agizo nyumba hizo zianze kupelekewa umeme lakini mpaka sasa bado hazina umeme.

Alilitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuwapelekea umeme wananchi hao ndani ya siku saba.

Pia, aliwaagiza Maafisa Uhusiano wa shirika hilo nchini kote, kuwahamasisha wananchi katika maeneo yao, kuweka umeme kwenye nyumba zao pamoja na kuwaelimisha kuhusu utaratibu wanaopaswa kufuata wakihitaji kuunganishiwa nishati hiyo.

Vilevile, aliwataka wananchi wa vijiji hivyo, kuanza mara moja kutafuta wataalamu wa kutandaza mfumo wa nyaya za umeme kwenye nyumba zao ili wapelekewe umeme kwa haraka.

Aidha, aliwataka



Moja ya nyumba ambazo Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani alizikagua kujua sababu za kutounganishiwa umeme hadi sasa. Waziri (hayupo pichani) alikuwa katika ziara ya kazi kijijini Usagara, Wilaya ya Misungwi, Mkoa wa Mwanza, Juni 26, 2020

wakandarasi wa umeme nchini kufanya kazi kwa weledi na kuonya kuwa kwa watakaoshindwa kutekeleza agizo hilo, watasimamishwa kazi mara moja na kupewa kazi hiyo wakandarasi wenye uwezo.

“Katika Mkoa huu wa Mwanza, tumemfuta kazi

mkandarasi aliyekuwepo na tumemweka mkandarasi mwingine. Tumempa hadi mwisho wa mwezi huu, awe amemaliza kazi,” alieleza Waziri.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Isamilo, Restuta Wilbard alikiri kufurahishwa na kitendo

hicho cha Waziri kukagua nyumba zao na kueleza kuwa imewapa hamasa kwenda kulipia huduma ya umeme na kwamba wako tayari kupokea huduma hiyo ambayo alisema itabadilisha maisha yao kwani itawawezesha kujajiri.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa kijiji cha Isamilo, Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza, akiwa katika ziara ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme vijijini, Juni 26, 2020



Wananchi wa kijiji cha Isamilo, Wilaya ya Misungwi, Mkoa wa Mwanza, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), wakati wa ziara yake kukagua kazi ya usambazaji umeme vijijini, Juni 26, 2020.

# Nguzo zitakazoharibika zibadilishwe kwa kuweka za zege - Kalemani

Zuena Msuya - Mara

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amesema kuwa kuanzia Septemba Mosi, 2020, nguzo yoyote itakayoharibika na kuanguka katika eneo lolote nchini, mbadala wake uwe nguzo ya zege.

Alisema hayo Juni 7, 2020, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini pamoja na kuwasha umeme katika vijiji vya Hunyali wilayani Bunda, Bukoba wilayani Musoma na Kerukerege wilayani Serengeti, Mkoa wa Mara.

Alisema kuwa nguzo za zege zinakaa zaidi ya miaka 100, hivyo kwa kutumia njia hiyo kutapunguza changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara kwa kisingizo cha kubadilisha nguzo katika baadhi ya maeneo hasa yaliyopo katika ardhi yenye maji mengi, na pia katika maeneo yanayochomwa moto kila wakati na kusababisha nguzo kuungua.

“Sasa hivi umeme haukatiki, na hakuna sababu ya kukatika kwa kuwa umeme upo mwingi na ziada, lakini kuna baadhi ya maeneo wamekuwa wakikata umeme mara kwa mara kwa kisingizio cha kubadilisha nguzo hasa maeneo korofi. Sasa tunaweka za zege; hizi haziungui wala kuoza na kuanguka. Hii ndiyo dawa pekee ya kuweka nguzo imara kumaliza tatizo hilo,” alisema Dkt. Kalemani.



Wakazi wa Kijiji cha Bukoba wilayani Musoma, Mkoa wa Mara wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) aliyefika katika kijiji hicho kuwasha umeme wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, Juni 7, 2020.

Kuhusu upatikanaji wa umeme katika visiwa vilivyopo katika ukanda wa ziwa Victoria, Dkt. Kalemani alisema kuwa vyote vitapelekewa umeme kwa kupitisha nyaya chini ya maji na tayari wameshaanza kupeleka katika kisiwa cha Ukerewe, kazi inayotarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Amewatoa hofu wakazi wa maeneo hayo kuwa hawajasahaulika na serikali iko katika hatua nzuri za kuendelea na utekelezaji wa kazi hiyo katika kila kisiwa, hivyo wawe wavumilivu kwa kuwa tayari tafiti zimefanyika na kiasi cha fedha kinachohitajika kinafahamika, kinachosubiriwa ni kuanza kwa utekelezaji wake.

“Visiwa vyote vinapelekewa umeme kwa kupitisha nyaya

chini ya ardhi na tayari tumeanza katika kisiwa cha Ukerewe. Tutafika visiwa vyote vya Tanzania. Huu ni mkakati madhubuti wa kuhakikisha kuwa visiwa vyote vinatumia umeme tunaouzalisha nchini. Wananchi wa maneo hayo vumilieni kidogo, kazi inafanyika,” alisisitiza Dkt. Kalemani.

Aliendelea kuwasisitiza wananchi wasisubiri nguzo bali waendeleo kulipia gharama za kuunganishiwa umeme ambayo ni shilingi 27,000 tu. Pia aliwaasa wasikubali kuuziwa nguzo, mita za LUKU wala nyaya, na watumie wakandarasi walioidhinishwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutandaza nyaya katika nyumba zao ili kuepuka vishoka na watu wasio waaminifu.

Aidha, Naibu Waziri

wa Nishati Subira Mgalu na Katibu Mkuu wa Wizara, Mhandisi Zena Said, ambao pia walishiriki ziara hiyo, waliwasha umeme katika shule ya msingi Bunyunyi. Pia, waliendesha harambee ya kuchangia mashine ya kutoa nakala kivuli (photocopy) katika shule hiyo iliyopo wilayani Bunda mkoani Mara.

Katika harambee hiyo zaidi ya shilingi milioni moja ilipatikana ambayo itanunua mashine ya kutoa nakala kivuli yenye thamani ya shilingi 900,000.

Ziara hiyo ilishia katika kijiji cha Kerukerege, wilayani Serengeti Mkoani Mara, ambapo baada ya kuwasha umeme katika kijiji hicho pamoja na mambo mengine, wakazi wa kijiji hicho walimsimika Waziri wa Nishati Dkt. Kalemani kuwa Chifu wa eneo hilo na kumpa jina la Dkt. Chacha Remu Kalemani.

Aidha, walitoa zawadi ya ng'ombe wawili, mmoja akiwa wa kwake na mwingine ampelekee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli.

Sambamba na hilo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, alipewa jina la Rhobi Kerongwe ikiwa ni heshima ya jina la mwanamke mzaliwa wa kwanza katika jamii hiyo pamoja na kumkabidhi zawadi ya mbuzi.

Wanakijiji hao walieleza sababu ya kuwazawadia viongozi hao ni kufuatia furaha yao kwa kuwa hao ni viongozi wa kwanza kufika katika eneo hilo tangu kuanzishwa kwa kijiji hicho.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemari (katikati) akipokea zawadi ya Kondoo kutoka wa wakazi wa Kijiji cha Hunyali, wilayani Bunda mkoani Mara, alipofika katika kijiji hicho kuwasha umeme wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, Juni 7, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (katikati) akipokea zawadi ya Kondoo kutoka wa wakazi wa Kijiji cha Hunyali, wilayani Bunda mkoani Mara, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemari kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, Juni 7, 2020.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (katikati) akipokea zawadi ya Kondoo kutoka wa wakazi wa Kijiji cha Hunyali, wilayani Bunda mkoani Mara, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemari kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, Juni 7, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemari (wa pili - kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Msafiri Mtemi (kushoto), na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati (wa pili - kulia) wakimsikiliza Diwani wa Kijiji cha Kerukerege (hayupo pichani), wakati wa ziara ya Waziri kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini katika Mkoa wa Mara Juni 7, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemari (aliyekaa), akisimikwa kuwa chifu wa kijiji cha Kerugerege wilayani Serengeti, Mkoa wa Mara na kupewa jina la Dkt. Chacha Remu Kalemari. Waziri alifika katika kijiji hicho kuwasha umeme akiwa katika ziara kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme katika Mkoa huo, Juni 7, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kulia) na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Zena Said (kushoto) wakiwa na fedha za kununua mashine ya kutoa nakala kivuli (photocopy) kwa ajili ya shule ya msingi Hunyanyu katika Kijiji cha Hunyali wilayani Bunda mkoani Mara, baada ya kuendesha harambee ya kuchangia mashinote hiyo, wakiwa katika ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini na kuwasha umeme katika baadhi ya vijiji vya Mkoa huo, Juni 7, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani (kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima walipofika kuwasha umeme katika Kijiji cha Bukoba, wilayani Musoma, wakati wa ziara yake ya kukagua maeneo ya usambazaji wa umeme katika Mkoa huo, Juni 7, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na Katibu Mkuu wa Wizara, Mhandisi Zena Said (kushoto), wakichangia fedha za kununua mashine ya kutoa nakala kivuli (photocopy) kwa ajili ya shule ya msingi Hunyanyu, katika kijiji cha Hunyali wilayani Bunda, Mkoa wa Mara, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini na kuwasha umeme katika baadhi ya vijiji vya Mkoa huo, Juni 7, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani (kulia) akipokea zawadi ya ng'ombe wake na wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, kutoka kwa wakazi wa kijiji cha Kerugerege, wilayani Serengeti, Mkoa wa Mara, alipofika kuwasha umeme katika kijiji hicho wakati wa ziara yake kukagua maeneo ya usambazaji wa umeme katika Mkoa huo, Juni 7, 2020.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said akipokea zawadi ya maboga kutoka kwa akina mama wa kijiji cha Kerugerege, wilayani Serengeti, Mkoa wa Mara. Wanawake hao walimpa Katibu Mkuu, jina la Rhobi Kerongwe, ikiwa ni heshima ya jina la mwanamke mzaliwa wa kwanza katika jamii hiyo. Tukio hilo lilifanyika wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani kukagua maeneo ya usambazaji wa umeme katika Mkoa huo, Juni 7, 2020.



Taswira ya nyumba ikiwa imefungiwa mita ya kupima matumizi ya gesi asilia kwa ajili ya kupikia. Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani alizindua ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo la Mnazi Mmoja mkoani Lindi, Mei 30, 2020.



Bomba la madini ya shaba lililofungwa ndani ya chumba cha jiko kwa ajili ya kuunganisha jiko la kupikia kwa kutumia gesi asilia. Hapa ni katika moja ya nyumba zilizopo eneno la Mnazi Mmoja wilayani na mkoani Lindi. Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani alizindua ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo hilo Mei 30, 2020.

## Wateja wa awali gesi asilia majumbani kuunganishwa bure

Zuena Msuya - Lindi

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amesema kuwa Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) itasambaza na kuunganisha bila malipo (bure) miundombinu ya gesi asilia kwa matumizi ya majumbani kwa wateja wa awali katika mikoa yote itakayofikiwa na huduma hiyo nchini.

Alisema hayo Mei 30 mwaka huu, wakati akizindua mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika Kijiji cha Mnazi Mmoja, mkoani Lindi na kuwataka wakazi wa eneo hilo kuchangamkia fursa hiyo ili kujiletea maendeleo na kuondokana na uchafuzi wa mazingira, gharama kubwa za kununua mkaa na kuni pamoja na adha ya kutafuta kuni porini kwa ajili ya kupikia.

Waziri aliweka wazi kuwa baada

ya kuunganishiwa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika nyumba zao, taasisi kama vile shule, hospitali au sehemu za biashara kama vile hoteli au migahawa, mteja atawekewa mita ya kupimia kiasi cha gesi anayotumia itakayofanya kazi kama LUKU za umeme.

Alisema baada ya kufungiwa miundombinu hiyo ya kusambaza gesi asilia, mteja atatakiwa kununua uniti za gesi kulingana na mahitaji yake kama ilivyo katika umeme, na endapo zitaisha kabla ya kuongeza nyingine, mita itajifunga hadi pale atakaponunua uniti nyingine kuingezea. Alisema mfumo huo unaitwa 'Malipo kabla ya Kutumia (Pre- Paid System)'

Akifafanua zaidi, Dkt. Kalemani alisema familia yenye wastani wa watu sita (6), inakadiriwa kutumia kiasi cha gesi ya shilingi 30,000 tu kwa mwezi kwa matumizi yote ya kupikia bila kubagua aina ya vyakula vinavyotumia muda

mrefu jikoni kama vile maharagwe.

"Watanzania wenzangu mnataka serikali iwape nini tena! Imegundua gesi asilia nchini kwetu inayotuzalishia umeme. Sasa tunasambaziwa gesi hii majumbani ili tuitumie kupikia vyakula vyetu na hatulipii chochote wakati wa kuunganishwa kwa hawa wateja wa awali. Zaidi, tutalipia kile tunachotumia na ni gharama ndogo mno ukilinganisha na matumizi ya kuni na mkaa. Nawahamasisha mjitokeze kwa wingi mfungwiwe gesi katika makazi yenu," alisema Dkt. Kalemani.

Vilevile, alieleza kuwa, serikali imeamua kufanya hivyo ili kuhamasisha matumizi ya gesi asilia iliyopatikana kwa wingi hapa nchini pamoja na kupunguza ukataji wa miti hovyoo kwa ajili ya kuni na kuchoma mkaa ili kusaidia juhudi za kutunza na kuhifadhi mazingira.

Alisema mradi wa usambazaji wa gesi asilia ni endelevu, ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 wateja wapya 2,000 wataunganishiwa

gesi majumbani ambapo 300 kati yao wanatoka Mkoa wa Lindi na vitongoji vyake. Waziri aliwapa faraja akina mama kuwa sasa wataondokana na adha ya kutembea porini kutafuta kuni.

Alitaja mikoa inayofuata katika utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kuwa ni pamoja na Morogoro, Dodoma na Singida.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio aliwatoa hofu watumiaji wa gesi asilia majumbani kuwa usanifu na ujenzi wa miundombinu hiyo, umezingatia hatua zote za usalama ili kuhakikisha matumizi ya gesi hiyo yanakuwa salama zaidi kwa mtumiaji na jamii kwa ujumla na hivyo kuwaomba wananchi kuondoa hofu katika matumizi ya nishati hiyo.

"Usalama wa gesi hii ni kutokana na tabia yake kwani ni nyepesi kuliko hewa tunayovuta, hivyo kama ikitokea imevuja basi hupotelea hewani mapema na haiwezi kulipuka wala kusababisha moto."

Aidha, alisema kuwa usambazaji wa gesi asilia ni salama zaidi kwa kuwa

## Wateja wa awali gesi asilia majumbani kuunganishwa bure

INATOKA UK.

15

husambazwa katika mgandamizo mdogo kwa njia ya bomba tofauti na gesi nyinyine. "Ni imani yangu kuwa wananchi wengi mtatumia gesi hii kwa kuwa ni salama zaidi na yenye gharama nafuu," alisema Dkt. Mataragio.

Akizungunzia gharama za matumizi ya gesi hiyo kwa familia yenye wastani wa watu watano hadi 6 ikilinganishwa na mkaa pamoja na kuni, Dkt. Mataragio alisema kuwa kwa wastani, gharama za matumizi ya mkaa kwa wiki siyo chini ya shilingi 4,500 wakati matumizi hayohayo kwa kutumia gesi ni shilingi 1,000 tu.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi alisema kuwa Mkoa wa Lindi umeandika historia nyingine iliyokuwa ikisubiriwa kwa muda mrefu ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia itakayokuwa ikitumika



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemari akikagua miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani katika baadhi ya mitaa ya eneo la Mnazi Mmoja, mkoani Lindi alipofanya uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu hiyo Mei 30, 2020.

kwa kupikia majumbani, mahotelini kwenye taasisi za afya, elimu na matumizi mengineyo kama viwandani na kuendesha magari.

Zambi aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Nishati na TPDC kwa kutenga fedha

zita kaweza utekelezaji wa mradi huo katika Mkoa wa Lindi na baadaye kote nchini. Aidha, aliwashukuru wana-Lindi kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote cha kutekeleza mradi huo na kuwaomba waendeleo na

moyo huo wa kizalendo.

"Wana-Lindi tuchangamkie fursa hii. Matumizi ya gesi asilia ni rahisi zaidi ukilinganisha na nishati aina yoyote ile. Mnajua wenyewe mnavyonunua mkaa bei ghali na kuhangaika kutafuta kuni porini huku mama na binti zetu wakiwa ndiyo waathirika wakubwa. Tujitokeze sasa kuunganishwa gesi ambayo ni bure kabisa," alisema Zambi.

Tukio hilo la uzinduzi wa gesi asilia, lilihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, baadhi ya Wabunge wa Mkoa wa Lindi, viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Nishati na taasisi zilizo chini yake pamoja na viongozi wa dini, vyama vya siasa na serikali wa Mkoa huo.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, kati ya futi za ujazo trilioni 57.54 za gesi asilia zilizogunduliwa nchini, kiasi cha futi za ujazo trilioni 1.3 zimetengwa kwa matumizi ya majumbani, viwandani, taasisi mbalimbali na kwenye magari. Kiasi hicho kitatumika kwa takribani miaka 30 ijayo.



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemari (katikati), akisikiliza maelezo ya namna mita ya kupima gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani, inavyofanya kazi, kutoka kwa mmoja wa wafanyakazi wa Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC), wakati wa hafla ya uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo la Mnazi Mmoja mkoani Lindi, Mei 30, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kushoto) na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Zena Said (kulia) wakiteta jambo wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani katika eneo la Mnazi Mmoja mkoani Lindi. Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemari alizindua ujenzi wa miundombinu hiyo Mei 30, 2020.





Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemami na Ujumbe wake (kulia) wakioneshwa ramani ya mtandao wa usambazaji wa miundombinu ya gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani kutoka katika visima vya kuchimba gesi, baada ya kuzindua ujenzi wa miundombinu hiyo katika eneo la Mnazi Mmoja mkoani Lindi, Mei 30, 2020.



Kutoka kushoto ni Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemami, Naibu Waziri Subira Mgalu na Katibu Mkuu, Mhandisi Zena Said, wakifuatilia ujumbe wa shairi uliokuwa ukitolewa na mmoja wa wanakijiji katika eneo la Mnazi Mmoja mkoani Lindi, wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo hilo Mei 30, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami (kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi (kushoto), wakiteta jambo wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo la Mnazi mmoja mkoani Lindi Mei 30, 2020.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio (katikati), akicheza na wakazi wa eneo la Mnazi Mmoja, mkoani Lindi kufurahia uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo hilo Mei 30, 2020.



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, akizungumza na wakazi wa eneo la Mnazi Mmoja wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo hilo Mei 30, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami akizungumza na wakazi wa eneo la Mnazi Mmoja mkoani Lindi wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo hilo Mei 30, 2020.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, akizungumza na wakazi wa eneo la Mnazi Mmoja mkoani Lindi wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo hilo Mei 30, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akizungumza na wakazi wa eneo la Mnazi Mmoja, Lindi, wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo hilo Mei 30, 2020.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Dkt. James Mataragio, akizungumza na wakazi wa eneo la Mnazi Mmoja mkoani Lindi, wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo hilo Mei 30, 2020.

# WAZIRI KALEMANI AIPONGEZA BODI YA TANESCO

Veronica Simba –  
Dodoma

**W**aziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ameipongeza Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), akisema imefanya kazi nzuri katika kushughulikia changamoto mbalimbali za umeme nchini.

Alibainisha hayo Juni 17, 2020 alipokutana na kuzungumza na Bodi hiyo jijini Dodoma, akiwa ameambatana na Naibu wake, Subira Mgalu, Katibu Mkuu Mhandisi Zena Said na viongozi wengine waandamizi wa Wizara.

Mojawapo ya kazi zilizotekelezwa na Bodi hiyo, ambazo Waziri anakiri kuridhishwa nazo, ni kushughulikia changamoto ya kukatika-katika kwa umeme katika maeneo mbalimbali nchini, ambayo amesema imetatuliwa kwa asilimia kubwa.

“Changamoto hiyo kwa sasa inatokea mara chache sana, na sababu yake



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati), akizungumza na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Juni 17, 2020 katika Ofisi za Wizara, Dodoma.

kuu ni matengenezo ya miundombinu ya umeme yanayokuwa yakifanyika katika eneo husika,” alifafanua Waziri na kuitaka Bodi hiyo iendelee kuhakikisha changamoto hiyo inatatuliwa kabisa.

Aidha, Dkt Kalemani aliipongeza Bodi hiyo kwa

kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji na usafirishaji wa umeme lakini akaitaka ihakikishe miradi inayoendelea kutekelezwa, inakamilika mapema ili kuwanufaisha wananchi.

Vilevile, aliisisitiza kuendelea kusimamia

mkakati wa kuiunganisha umeme wa gridi migodi yote ya madini nchini ili kuwawezesha wachimbaji kufanya kazi hiyo kwa tija kwa manufaa yao na ya Taifa.


Katika hatua nyingine, Waziri aliitaka Bodi hiyo kuendelea kubuni mikakati mbalimbali itakayowezesha kuongeza idadi ya wateja wanaounganishiwa umeme kwa mwaka ili kuongeza mapato kwa shirika hilo.

Sambamba na hilo, aliwataka pia kufuatilia na kutafutia ufumbuzi wa kudumu changamoto ya upotevu wa umeme na kuhakikisha umeme wote unaotumika unalipiwa na wahusika.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Mwenyekiti wa Bodi hiyo Dkt. Alexander Kyaruzi, alimshukuru Waziri kwa Imani aliyoionesha katika utendaji wao na kumhakikishia kuwa watafanyia kazi maelekezo yote aliyowapa.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme Tanzania -TANESCO (hawapo pichani), Juni 17, 2020 katika Ofisi za Wizara, Dodoma. Kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara, Mhandisi Zena Said.



Baadhi ya Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na viongozi waandamizi wa Wizara, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemari (hayupo pichani), alipokutana nao kuzungumzia masuala mbalimbali ya kiutendaji, Juni 17, 2020 katika Ofisi za Wizara, Dodoma.

# TANESCO WATAKIWA KULIPA FIDIA KWA WANANCHI WA KIDAHWE

Hafsa Omar - Kigoma

**W**aziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemami ametoa siku tano kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kulipa fidia kwa wananchi wa Kidahwe, Kigoma Vijijini, mkoani Kigoma, waliopisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme.

Alitoa agizo hilo Juni 27, 2020, wakati akizindua kuanza malipo kwa wananchi ambao wameridhia kutoa ardhi yao kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha kupoza umeme cha Kidahwe.

Akizungumza kwenye tukio hilo, Waziri alisema kuwa, zaidi ya shilingi milioni 700 zipo tayari kwa ajili ya malipo ya wananchi 411 na kuitaka TANESCO kuanza mara moja kuwalipa wananchi hao.

"Niliacha maelekezo kwa waatalamu wetu kufanya kazi mbili, kazi ya kwanza ilikuwa kuhakikisha wananchi ambao wanapitiwa na mradi, wafanyiwe



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemami akisaini kitabu cha wageni alipofika kukagua ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nguruka, Kilichopo katika kijiji cha Mganza, Wilaya ya Uvinza, mkoani Kigoma, Juni 27, 2020.

tathmini na kulipwa fidia zao. Jambo hili tayari limeanza kufanyiwa kazi. La pili ni kuanza matayarisho ya ujenzi wa mradi huu mkubwa," alisema Dkt Kalemami.

Aidha, Waziri aliwashukuru wananchi wa eneo hilo kwa kutoa maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho

kikubwa chenye uwezo wa kuzalisha umeme wa kilovoti 400, ambao unatarajiwa kuondoa kero ya upatikanaji wa umeme mkoani humo.

Aliwataka wananchi watakaolipwa fidia hiyo kuzitumia vizuri fedha zao kwa kununua maeneo mengine na kujiendeleza kiuchumi.

"Mtakaolipwa fedha zenu, msije mkazitumia vibaya halafu mkarudi tena TANESCO kudai hela nyingine. Hakuna hela nyingine. Ni hiyohiyo mtakayolipwa," alisema. Vilevile, alilitaka

INAENDELEA UK.

21



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemami (kulia) akitoka kukagua ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nguruka, Kilichopo katika kijiji cha Mganza, Wilaya ya Uvinza, mkoani Kigoma, Juni 27, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemami akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kidahwe, Kigoma Vijijini, mkoani Kigoma, akiwa kwenye uzinduzi wa kuanza malipo kwa wananchi ambao wameridhia kutoa ardhi yao kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe, Juni 27, 2020.

# TANESCO WATAKIWA KULIPA FIDIA KWA WANANCHI WA KIDAHWE



Wananchi wa kijiji cha Kidahwe, Kigoma Vijijini, Mkoa wa Kigoma, wakifurahi mara baada ya Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemari (hayupo pichani), kuwatangazia kuwa ndani ya siku tano wote watakuwa wamelipwa malipo yao, kufuatia kutoa ardhi walizokuwa wakimiliki ili kupisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidahwe. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi, Juni 27, 2020.

INATOKA UK.

20

shirika hilo la ugavi wa umeme, kuanzia Julai 5 mwaka huu, lianze mara moja ujenzi wa kituo hicho, ili wananchi wa Kigoma waanze kupata

umeme wa uhakika ambao utawasaidia kujenga uchumi wa Mkoa huo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Emmanuel Maganga, aliwashukuru wananchi wote waliotoa maeneo yao kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa huo

na aliwahakikishia kuwa pesa za malipo yao ziko tayari.

Pia, aliwatahadharisha wale wote watakaolipwa fidia kuwa hawataruhusiwa kuyatumia tena maeneo hayo kwani yatakuwa ni mali ya Serikali.

Katika ziara hiyo, Waziri Kalemari pia alikagua kituo cha kupoza umeme cha Nguruka kilichopo katika kijiji cha Mganza na kuelekeza TANESCO kumaliza ujenzi wa kituo hicho Julai mwaka huu.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemari (kushoto) akiwa pamoja na Uongozi wa Mkoa wa Kigoma na baadhi ya wananchi wa kijiji cha Kidahwe, wakiwa wameshika mfano wa hundi itakayolipwa kwa wananchi wa kijiji hicho kilichopo kata ya Kidahwe, Kigoma Vijijini, Juni 27, 2020. Malipo hayo ni kufuatia kutoa ardhi walizokuwa wakimiliki ili kupisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidahwe.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemari (wa pili kutoka kushoto), akifurahi na baadhi ya wananchi baada ya kuzindua kuanza kwa malipo ya wananchi ambao wameridhia kutoa ardhi yao kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe, Juni 27, 2020.

# TPDC yaanza kurejeshewa mali zake zilizo milikiwa kiholela

Zuena Msuya –  
Dar es Salaam

**K**atibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said amewataka watu wote wanaomiliki mali za serikali kinyume na sheria na utaratibu wazirudishe katika mamlaka husika ili ziwanaufaishe watanzania wote na serikali kwa ujumla.

Mhandisi Zena alisema hayo, Juni 02, 2020, wakati wa makabidhiano ya Maghala matatu kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) yaliyokuwa yametwaliwa na kumilikiwa kinyume cha utaratibu na kampuni ya SACCOSSA kuanzia mwaka 2006.

Alisema hayo ni matokeo ya Tume iliyoundwa na TPDC kuhakiki mali zake, pia ni muendelezo wa zoezi la kurudisha mali za serikali zilizotwaliwa au



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, akizungumza na vyombo vya habari, Juni 2, 2020, wakati wa kukabidhi maghala ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), yaliyokuwa yametwaliwa na kampuni ya SACCOSSA tangu 2006.

kumilikiwa kinyume na utaratibu wa kisheria ili zirudishwe serikalini katika mamlaka husika.

Maghala hayo yaliyorudishwa kwa TPDC, yapo katika eneo la Mikocheni jijini Dar es salaam, ambapo ilielezwa kuwa, awali, Kampuni ya SACCOSSA iliingia makubalino na TPDC kuyatumia maghala hayo katika shughuli zake lakini baadaye kampuni hiyo ilienda kinyume na makubaliano ya mkataba kwa kutokulipa fedha ya pango huku ikiendelea kuyamiliki na kuyatumia majengo hayo pasipo kunufaisha mamlaka husika na serikali kwa ujumla.

“Baadhi ya watu hujimilikisha mali za serikali kiujanja-ujanja kwa muda mrefu huku serikali ikiwa haifaidiki. Sasa, kuna haja ya kurudisha mali hizo serikalini, moja baada ya nyingine. Jana

tu tumeshuhudia mali za mkonge zikirudishwa kule Tanga. Sisi leo tunarudisha hizi za TPDC na siyo hizi tu, tutarudisha mali zote za Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini yake. Natao wito kwa yeyote anayemiliki mali kinyume na taratibu aanze kuzirejesha mwenyewe,” alisema Katibu Mkuu.

Akizungumzia makubalino kati ya TPDC na SACCOSSA, Mhandisi Said alisema kuwa kampuni ya SACCOSSA ilikuwa mpangaji katika majengo hayo kuanzia miaka ya 2000 na walikuwa wakulipa pango vizuri kwa mujibu wa mkataba lakini ilipofika mwaka 2006, kampuni hiyo iliacha kulipa fedha hiyo ya pango huku wakiendelea kuyamiliki na kuyatumia bila kulipa chochote kwa zaidi ya miaka 10 hivyo kuleta mgogoro baina yao. Alifafanua kuwa, baada

INAENDELEA UK.

23



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio, akionesha hati ya makabidhiano ya kurudishwa kwa maghala matatu ya shirika hilo, yaliyokuwa yametwaliwa na Kampuni ya SACCOSSA kwa zaidi ya miaka 10, tangu 2006. Tukio hilo lilifanyika Juni 02, 2020 jijini Dar es Salaam.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (katikati), Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio (kulia) na Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa TPDC, George Seni, wakikagua maghala ya shirika hilo yaliyokuwa yametwaliwa na Kampuni ya SACCOSSA tangu 2006 ambayo kwa sasa yamerudishwa TPDC. Tukio hilo lilifanyika Juni 02, 2020 jijini Dar es Salaam.

## TPDC yaanza kurejeshewa mali zake zilizomilikiwa kiholela

INATOKA UK.

22

ya usuluhishi wa mgogoro huo, na TPDC kushinda kesi, SACCOSSA iliamuliwa kurejeshwa majengo hayo ili yatumiwe na mamlaka husika.

Katibu Mkuu aliagiza kampuni hiyo kulipa fedha za pango walizokuwa hawalipi katika kipindi chote hicho.

“SACCOSSA lazima mlipie fedha mnazodaiwa kwa mujibu wa makubaliano hata kama mmerudisha jengo hili. Serikali hii ina mali nyingi sana lakini wajanja wachache wamekuwa wakizitumia kwa faida zao binafsi na serikali hainufaiiki. Zoezi hili litaendelea nchi nzima. Lazima watazania wote wanufaike na wajivunie mali za serikali yao,” alisisitiza Mhandisi Said.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio, alisema kuwa,



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio (katikati) na Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa TPDC, George Seni (kushoto), wakikagua rasilimali ya vitu vilivyokuwepo katika maghala ya shirika hilo, yaliyokuwa yametwaliwa na Kampuni ya SACCOSSA tangu 2006 ambayo kwa sasa yamerudishwa TPDC. Tukio hilo lilifanyika Juni 2, 2020 jijini Dar es Salaam.

urudishwaji wa majengo hayo ni matokeo ya maagizo na maelekezo ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli, ya kutaka mali zote za serikali ambazo umiliki wake haufahamiki au kuhamishiwa kwa watu wengine bila kufuata

taratibu zihakikiwe na kurudishwa serikalini katika mamlaka husika.

Dkt. Mataragio alisema kuwa baada ya maagizo hayo iliundwa timu ya ndani ya kuhakiki mali zote za shirika hilo na kufanya kazi nzuri iliyotoa

taarifa iliyoainisha mali za shirika hilo inazozimiliki kisheria, zisizomilikiwa kisheria pamoja na zile zenye migogoro na kuanza kuzishughulikia.


“Tume hii iliyoundwa imefanya kazi nzuri sana. Tunaendelea kufanyia kazi taarifa iliyoletwa na Tume hiyo kwa utekelezaji wenye manufaa kwa shirika na Taifa kwa ujumla. Nawahakikishia kuwa mali zote za TPDC zitaendelea kuwa salama na katika umiliki sahihi kwa faida yetu sote watazania. Hili ni shirika letu, lazima Watazania tujivunie,” alisema.

Naye mwakilishi wa kampuni ya SACCOSSA, Donashan Kambamba alisema kuwa, kampuni hiyo iliridhia kuundwa kwa Tume husika na kukubali taarifa ya matokeo ya Tume hiyo pamoja na kuridhia kurejeshwa jengo hilo kwa mamlaka husika.

Kuhusu kulipa fedha wanazodaiwa kama walivyoagizwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, Kambamba alisema kuwa watakaa na kukubaliana na TPDC kuona namna bora ya kutekeleza agizo hilo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio (kulia), akikabidhi hati ya makubaliano ya kurudisha maghala matatu ya shirika hilo kwa mwakilishi wa Kampuni ya SACCOSSA, Donashan Kambamba. Maghala ya TPDC yalitwaliwa na Kampuni ya SACCOSSA kwa zaidi ya miaka 10, tangu 2006. Tukio hilo lilifanyika Juni 02, 2020 jijini Dar es Salaam.



Mwonekano wa majengo ya maghala ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), yaliyokuwa yametwaliwa na Kampuni ya SACCOSSA tangu 2006, ambayo kwa sasa yamerudishwa TPDC. Tukio hilo la kurudishwa kwa majengo hayo lilifanyika Juni 2, 2020 jijini Dar es Salaam.

# Nishati yafanya ukaguzi wa usalama katika maghala ya mafuta na gesi



Mashine ya kusukuma maji katika maghala ya kuhifadhi na kupakua mafuta. Kamishna wa Petroli na Gesi Adam Zuberi na Ujumbe wake, kuanzia Mei 26 hadi Juni 3, 2020 walifanya ziara ya kukagua juhudi zinazofanywa katika kakabiliana na usalama wa maghala hayo pindi ajali za moto zinapotokea

mapungufu yaliyopo katika Kampuni mbalimbali ili kukabiliana na majanga kama hayo.

Baada ya kufanya ukaguzi huo, walibaini changamoto mbalimbali hivyo Wizara ilizitaka Mamlaka husika kuruhusu kampuni hizo kuunganisha maji kutoka baharini pamoja na kuwa na mwongozo wa pamoja kuunganisha miundombinu ya maji na viwanda vilivyopo jirani ili kuweza kupata msaada kutoka kwa majirani wanaowazunguka katika kukabiliana na janga la moto pindi litakapotokea.

Aidha, Ujumbe huo ulishauri kuwepo na vikao vya pamoja baina ya kampuni hizo kwa lengo la kujadili masuala ya usalama na kuweka mikakati ya pamoja katika kukabiliana na majanga ya moto na mengine.

Kwa upande wao, wamiliki wa maghala waliomba Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka husika kuboresha mfumo wa gharama kubwa za kufanya tathmini ya athari kwa mazingira na kuwa rafiki kwa wawekezaji ili waweze kujenga kwa utaratibu unaotakiwa, tofauti na sasa ambapo mchakato huwa mrefu na

**Zuena Msuya –  
Dar es Salaam**

**W**izara ya Nishati imefanya ukaguzi wa kuangalia hali ya usalama katika maghala ya kuhifadhi na kupakua mafuta na gesi yaliyopo jijini Dar es salaam pamoja na kujionea tahadhali zinazochukuliwa katika maghala hayo ili kukabiliana na majanga ya moto endapo yakitokea.

Ukaguzi huo ulifanyika kwa muda wa wiki nzima kuanzia Mei 26 hadi Juni 3, 2020 ukiongozwa na Kamishna wa Petroli na Gesi kutoka Wizara ya Nishati pamoja maafisa wengine wa Wizara, kwa kushirikiana na maafisa kutoka Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) pamoja na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA).

Wizara ilifanya ukaguzi huo ili kutathmini mwenendo wa utekelezaji wa mapendekezo ya kamati iliyoundwa na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni kuchunguza chanzo cha

ajali ya moto ulitokea katika ghala la kuhifadhi mafuta na gesi, mali ya kampuni ya Lake Oil katika eneo la Kigamboni, mwanzoni mwa Januari 2020 pamoja na kubaini



Moja ya sehemu ya kupima mafuta (flow meter) yanayopakuliwa kutoka baharini kuingia katika maghala ya kuhifadhi na kupakua mafuta. Kamishna wa Petroli na Gesi Adam Zuberi na Ujumbe wake, kuanzia Mei 26 hadi Juni 3, 2020 walifanya ziara ya kukagua juhudi zinazofanywa katika kakabiliana na usalama wa maghala hayo pindi ajali za moto zinapotokea.



# Nishati yafanya ukaguzi wa usalama katika maghala ya mafuta na gesi

INATOKA UK.

24

wa gharama kubwa.

Alisema jambo hilo linalowafanya wawekezaji wengi kujenga bila kufanya tathmini ya athari ya mazingira na baadaye kujikuta wamekosa ushauri wa kitaalam unaohitajika kuzingatia kabla ya kujenga.

Wizara ilishauri Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuratibu mazoezi ya pamoja na kampuni za mafuta na gesi yanayolenga kujiandaa kupambana na majanga ya moto pamoja na kuanzisha kituo kikubwa cha jeshi hilo kwa upande wa Kigamboni.

Sambamba na hilo, EWURA ilishauriwa kuratibu vikao vya Usalama vitakavyofanyika kila mwezi vikijumuisha kampuni zote za mafuta na gesi pamoja na kufupisha muda wa upatikanaji wa leseni na kuvutia uwekezaji.

Kwa upande wa



Kamishna wa Petroli na Gesi wa Wizara ya Nishati, Adam Zuberi (katikati) akikagua moja ya pampu za maji zinazotumika kuzima moto katika maghala ya kuhifadhi na kupakua mafuta pindi majanga ya moto yanapotokea. Kamishna na Ujumbe wake, kuanzia Mei 26 hadi Juni 3, 2020 walifanya ziara ya kukagua juhudi zinazofanywa katika kakabaliana na usalama wa maghala hayo pindi ajali za moto zinapotokea.

Kampuni, zilishauriwa kuwa na maeneo maalumu na ya kutosha kwa ajili ya maegesho ya magari yanayosubiri kujaza mafuta ili kupunguza msongamano.

Aidha, Mamlaka husika zilishauriwa kuweka mwongozo wa bei elekezi

ya Serikali kwa ajili ya fidia za makazi yaliyopo jirani na maghala ya kuhifadhi mafuta na gesi ili waondolewe katika maeneo hayo kupunguza athari zinazoweza kutokea endapo janga la moto litatokea.

Ujumbe huo wa Wizara

pia ulizishauri kampuni zote hususan za wazawa kuajiri maafisa wa afya na usalama kazini ili pamoja na kusimamia shughuli za usalama kazini waweke mpango mkakati wa mafunzo yanayohusu namna bora ya kukabiliana na majanga na kunda mpango shirikishi wa kufanya mazoezi ya dharura ili kujiandaa nyakati za majanga kama hayo.

Pia, ilishauriwa kampuni hizo kuwa na utaratibu wa kufanya matengenezo ya kudumu ya miundombinu na ukaguzi wa kiufundi wa mara kwa mara katika maghala yao ili kuwezesha miundombinu hiyo kudumu na kuwa imara wakati wote.

Aidha, Kamati hiyo ilitembelea kampuni za Lake Oil Limited, TIPER, World Oil Limited, Sahara Tanzania Limited, GBP, PUMA, Total, Manjis Gas, Afroil Investment Limited, TAZAMA, Camel Gas, Oryx Gas Limited pamoja na Hass Petroleum (T) Limited.



Kituo cha mafuta kikiwa kinamwaga maji kwa njia ya kisasa, kuonesha namna ambavyo wanaweza kukabiliana na majanga ya moto pindi yanapotokea. Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi na Ujumbe wake, walifanya ziara kuanzia Mei 26 hadi Juni 3, 2020 kukagua juhudi zinazofanywa katika kakabaliana na usalama wa maghala ya kuhifadhi na kupakua mafuta, pindi ajali za moto zinapotokea.



Tanki la kuhifadhi gesi likimwaga maji kwa njia ya kisasa, kuonesha namna ambavyo wanaweza kukabiliana na majanga ya moto pindi yanapotokea. Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi na Ujumbe wake, walifanya ziara kuanzia Mei 26 hadi Juni 3, 2020 kukagua juhudi zinazofanywa katika kakabaliana na usalama wa maghala ya kuhifadhi na kupakua mafuta, pindi ajali za moto zinapotokea.

# Katibu Mkuu Nishati akagua uzalishaji wa gesi asilia



Meneja Mkuu wa Kampuni ya Gesi (GASCO) ambayo ni Kampuni Tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Mhandisi Baltazar Mroso (katikati) akitoa maelezo kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (mwenye ushungi) kuhusu namna gesi asilia inavyosafirishwa. Katibu Mkuu alikuwa katika ziara kukagua mradi wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Mei 30 - Juni 1, 2020.

## Zuena Msuya - Mtwara

**K**atibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said amefanya ziara ya kutembelea na kukagua miundombuni ya uchimbaji, uchakataji na usafirishaji wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mhandisi Zena alifanya ziara hiyo Mei 30 na Juni 1, 2020 kwa kukagua visima vya kuchimba gesi vilivyopo Mnazi Bay eneo la Msimbati, kiwanda cha kuchakata gesi hiyo cha Madimba mkoani Mtwara na Kituo cha kupokea gesi na kufua umeme cha Somanga Fungu mkoani Lindi.

Lengo la ziara hiyo lilikuwa kujionea utendaji kazi wa mfumo mzima wa uchimbaji, uchakataji, usafirishaji wa gesi asilia na kufua umeme pamoja na matumizi mengine ya majumbani, mahotelini,

viwandani na kwenye magari.

Baada ya kukagua na kuona ufanyaji kazi wa mfumo huo, alilipongeza Shirika la Maendeleo ya



Meneja Mkuu wa Kampuni ya Gesi (GASCO) ambayo ni Kampuni Tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Mhandisi Baltazar Mroso (katikati) akimuonesha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (mwenye ushungi), mita ya kupima kiwango cha gesi asilia inavyosafirishwa kupitia vituo vya usalama na dharura. Katibu Mkuu alikuwa katika ziara kukagua mradi wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Mei 30 - Juni 1, 2020. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio.

Petroli Tanzania (TPDC) kwa kuendelea kufanya kazi kwa weledi na uzalendo mkubwa.

“Huu ni mradi wetu sisi watanzania ambao tunajivunia kuwa nao. Hongereni sana TPDC, mnaifanya kazi nzuri inayoonekana. Watanzania pia wanafahamu juu ya kazi yenu.”

Alisema kuwa uzalendo ni jambo la msingi kwa kila Taifa ili liweze kuthamini vitu vyake vya ndani na kusonga mbele hivyo akawataka wataalam kusimama imara kwa maslahi mapana ya Taifa.

Aidha, aliliagiza shirika hilo, kuendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wataalam wa mradi huo ili kuwajengea uwezo zaidi wa kitaaluma katika kukabiliana na ukuaji teknolojia unaobadilika duniani kila siku.

Vilevile, alitoa wito kwa wataalam hao

kutokubali kurubuniwa kwa namna yoyote ile, na kwa wale wakongwe na wenye uzoefu wa muda mrefu katika utekelezaji na usimamizi mradi huo, aliwataka wasiwe wanyimi bali wawarithishe uzoefu na ujuzi zaidi vijana ambao ni wapya katika taaluma hiyo.

Aliwapongeza kwa kuendelea kutunza mazingira yanayozunguka mradi huyo uliodumu kwa miaka mitano sasa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji TPDC, Dkt. James Mataragio alieleza kuwa mbali ya kuwepo kwa tishio la virusi vya Corona nchini, uzalishaji wa gesi asilia haukuathirika badala yake uliendelea kuongezeka kutoka futi za ujazo milioni 60 hadi kufikia futi za ujazo milioni 90.

“Corona haikuathiri kabisa uchimbaji na uzalishaji wa gesi asilia hapa nchini. Tumeendelea kufanya kazi huku tukichukua tahadhari kwa kuzingatia maelekezo ya wataalam wa afya.”

Alisema kuwa uzalishaji wa gesi hadi kufikia Aprili 2020, ulifikia futi za ujazo milioni 90, na kwamba sehemu ya umeme unaozalishwa sasa unatumia gesi hiyo.

Hii ni mara ya kwanza kwa Katibu Mkuu kutembelea mradi huo wa gesi, tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo na Mheshimiwa Rais John Magufuli, mapema mwaka huu.

Katibu Mkuu pamoja na Ujumbe wake, walitembelea pia kiwanda cha kutengeneza marumaru pamoja cha GoodWill kilichopo wilayani Mkuranga mkoani Pwani kinachotumia gesi asilia inayochimbwa hapa nchini kuendesheba shughuli zake za uzalishaji.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (mwenye ushungi) akikagua bomba la kusafirisha gesi, alipotembelea moja ya vituo vya usalama na dharura vya kusafirisha gesi asilia. Katibu Mkuu alikuwa katika ziara kukagua mradi wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Mei 30 - Juni 1, 2020. Kushoto ni viongozi waandamizi wa wizara na taasisi zake alioambatana nao katika ziara hiyo.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (wa pili-kulia), akitoa maelekezo kwa msimamizi wa eneo linalochimbwa gesi asilia la Mnazi Bay, Msimbati, alipotembelea moja ya vituo vya usalama na dharura vya kusafirisha gesi asilia. Katibu Mkuu alikuwa katika ziara kukagua mradi wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Mei 30 - Juni 1, 2020.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (katikati) akisikiliza maelezo ya namna mtambo wa kuunguza gesi kwa ajili ya usalama (haupo pichani) unavyofanya kazi, kutoka kwa Meneja wa Kiwanda cha kuchakata Gesi cha Madimba, Mhandisi Sultan Pwaga, (aliyenyoosha mkono). Katibu Mkuu alikuwa katika ziara kukagua mradi wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Mei 30 - Juni 1, 2020.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (katikati) pamoja na viongozi waandamizi wa Wizara na Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC), wakikagua mitambo ya kiwanda cha kuchakata gesi asilia cha Madimba mkoani Mtwara. Katibu Mkuu alikuwa katika ziara kutembelea mradi wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Mei 30 - Juni 1, 2020.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (katikati) akizungumza na mmoja wa wataalam wanaosimamia chumba cha kuendesha mitambo kwa kutumia teknolojia maalum (Control Room) katika kiwanda cha kuchakata gesi asilia cha Madimba mkoani Mtwara. Katibu Mkuu alikuwa katika ziara kukagua mradi wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Mei 30 - Juni 1, 2020.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (katikati) akioneshwa mitambo ya Kituo cha kupokea gesi na kufua umeme cha Somanga Fungu mkoani Lindi, wakati wa ziara yake kukagua mradi wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Mei 30 - Juni 1, 2020. Kushoto kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio na kulia kwake ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya Gesi (GASCO) ambayo ni Kampuni Tanzania ya TPDC, Mhandisi Baltazar Mroso.

## REA III mzunguko wa kwanza itakamilika kwa wakati – BODI



### Zuena Msuya - Dodoma

**W**ajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wameridhishwa na maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme vijijini, awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza na kusema kuwa mradi huo utakamilika kwa wakati. Mwenyekiti wa Bodi, Wakili Julius Kalolo, aliyasema hayo Juni 17 mwaka huu, jijini Dodoma, wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemami na Bodi hiyo kujadili maendeleo ya utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini.

Katika kikao hicho, pamoja na mambo mengine, Waziri alikiri kuridhishwa na hatua

zilizofikiwa juu ya utekelezaji wa REA III mzunguko wa kwanza na kusema kuwa ana imani mradi huo utakamilika kama ulivyopangwa.

Aliitaka Bodi hiyo kuendelea kufanya kazi yake kwa weledi kwa kuzingatia maslahi ya Taifa.

Vilevile, aliipongeza Bodi hiyo kwa kazi nzuri iliyofanya, na kuitaka kuendelea kutoa ushauri juu ya miradi inayoendelea.

Dkt. Kalemami alisema aliitisha kikao hicho kwa lengo la kujadiliana na Wajumbe wa Bodi hiyo ili kuafikiana namna nzuri zaidi ya kuboresha utekelezaji wa miradi inayoendelea ili kuondokana na changamoto zilizojitokeza katika miradi iliyotangulia.

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami, (katikati), akizungumza wakati wa kikao chake na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati vijijini (REA) alipokutana nao Juni 17, 2020, Dodoma. Kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara, Mhandisi Zena Said.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemami (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati vijijini (REA) baada ya kikao chao kilichofanyika Juni 17, 2020, Dodoma. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na kulia kwake ni Katibu Mkuu wa Wizara, Mhandisi Zena Said.

# ZIARA KUKAGUA MIRADI YA REA MOROGORO YALETA NEEMA KWA WANANCHI



Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga akizungumza wakati Timu ya Wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zake, ilipofanya kikao na wananchi wa Vidunda, Morogoro, kujadili maendeleo ya Mradi wa Umeme Vijijini katika eneo hilo, Juni 25, 2020.

## Veronica Simba

Ziara ya Timu maalumu ya wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zake zinazohusika na umeme, kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini mkoani Morogoro imeleta neema kwa wananchi husika.

Timu hiyo inayoongozwa na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga imefanikisha kuwashwa umeme katika vijiji nane hadi sasa huku kazi ya kuvifikia vijiji vingine zaidi ikiendelea.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii, Juni 25, 2020, Mhandisi Luoga alisema ziara hiyo ya siku saba ilianza Juni 22 mwaka huu ikilenga kutatua changamoto zinazomkabili Mkandarasi anayetokeleza mradi husika mkoani humo,

ambaye ni kampuni ya State Grid Engineering.

“Kazi yetu ni kutatua changamoto zinazomkabili Mkandarasi ili kuharakisha utekelezaji wa Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza, uweze kukamilika kwa wakati, mwishoni mwa mwezi huu,” alifafanua Luoga.

Katika kufanikisha azma hiyo, Mhandisi Luoga alieleza kazi zilizofanywa na timu hiyo hadi sasa ni kufanya vikao na viongozi mbalimbali wa serikali akiwemo Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Watendaji wa Kata na Wenyeviti wa Vijiji ili kusikiliza changamoto za wananchi katika utekelezaji wa Mradi.

Akielezea changamoto hizo, Luoga alisema timu yake imeshuhudia orodha ndefu ya wananchi waliolipia huduma za kuunganishiwa

umeme lakini walikuwa hawajapewa huduma hiyo.

Nyingine ni uwepo wa nguzo zilizosimamishwa pasipo kuvutiwa nyaya pamoja na ukosefu wa mita na transfoma.

“Hivi ninavyoongea tumeshawasha umeme katika vijiji nane vya Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi na tunaendelea na zoezi hilo katika Wilaya za Gairo, Mvomero, Kilosa na Morogoro Vijijini,” alieleza.

Alivitaja vijiji hivyo kuwa ni Michenga, Ihanga, Ideuindembo, Ipugusa, Sali, Mtukula, Namgezi na Msogezi.

Akifafanua Zaidi, Mhandisi Luoga alisema hadi kukamilika kwa ziara jumla ya vijiji 25 vitawashiwa umeme.

Kuhusu changamoto ya upatikanaji wa vifaa, Mhandisi Luoga alieleza kuwa kwa kushirikiana

na Mkandarasi, Timu yake imeweza kutatua changamoto hiyo ambapo nyaya, mita na transfoma zimepatikana.

Katika hatua nyingine, Mhandisi Luoga alizungumzia mkakati wa Serikali kujenga kituo cha kupoza umeme Ifakara ambacho alisema kikikamilika kitasaidia kuboresha upatikanaji wa nishati hiyo katika maeneo ya Kilombero, Ifakara, Ulanga na Malinyi.

Alisema ujenzi wa Kituo hicho utagarimu takribani shilingi bilioni 23 za Tanzania, ambazo ni fedha za Serikali pamoja na misaada ya wafadhili wa Serikali ya Ulaya.

Timu hiyo ya Wataalamu ilijumuisha pia Naibu Mkurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania, Mhandisi Raymond Seya, Afisa kutoka Wizara ya Nishati anayesimamia miradi ya Umeme Vijijini, Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Stephan Kashushura, Mafisa wanaosimamia Mradi huo kutoka TANESCO na REA pamoja na Mkandarasi anayetokeleza Mradi husika, kampuni ya State Grid Engineering.



Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga akizungumza wakati Timu ya Wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zake, ilipofanya kikao na Wakandarasi kutoka Kampuni ya AEE Power na Burhani Engineers, wanaotekeleza Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Ifakara, mkoani Morogoro, Juni 25, 2020 wakiwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme.

# MIAKA MITANO YA MAFANIKIO SEKTA YA NISHATI

Na Veronica Simba

**K**wa mujibu wa Kamusi mbalimbali, neno mafanikio linaelezwa kuwa ni kufikia malengo uliyojiwekea ndani ya muda uliopanga au kufanya jambo likaleta matokeo mazuri, lakini pia, mafanikio yanapimwa kuwa ni kinyume cha kushindwa.

Tafsiri hizo zote zinasadifu hali halisi iliyopo katika sekta ya nishati. Kwa lugha rahisi, ni kwamba, sekta ya nishati imekuwa na mafanikio katika nyanja mbalimbali, ambayo kwayo Watanzania wana kila sababu ya kujivunia.

Makala hii, inaangazia mafanikio ya sekta ya nishati ndani ya kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Rais John Joseph Pombe Magufuli, ambaye kwakweli utendaji wake mahiri umekuwa ni gumzo ndani na nje ya nchi.

Ni kutokana na uongozi huo ninaothubutu kusema umetukuka, ndiyo umewawezesha hata wasaidizi wake aliowateua kusimamia sekta ya nishati, kufanya kazi kwa weledi, maarifa na kujituma hivyo kuwezesha mafanikio ninayoyazungumzia katika andiko hili.

Viongozi hao wakiongozwa na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, Naibu Waziri Subira Mgalu, Katibu Mkuu Mhandisi Zena Said, Naibu Katibu Mkuu



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akimuwashia umeme Veronica Maghembe (mwenye mtoto mgongoni), mkazi wa kijiji cha Bigegu, wilayani Bunda, Mkoa wa Mara ikiwa ni ishara ya kuwasha rasmi umeme katika kijiji hicho, Novemba 18, 2019.

Mhandisi Leonard Masanja na viongozi wengine wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake, wamewezesha sekta ya nishati kufikia mafanikio makubwa.

Nishati imegawanyika katika sekta ndogo kuu mbili ambazo ni umeme na ile ya mafuta na gesi. Hivyo basi, nitadadavua mafanikio husika katika mgawanyo wa sekta hizo ndogo.

Umeme Upane wa umeme, kumekuwa na mafanikio ya kujivunia katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano. Miongoni

mwa mafanikio hayo ni kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme nchini ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini umeongezeka na kufikia jumla ya megawati 1,601.84 kutoka megawati 1,308 mwaka 2015.

Mafanikio mengine ni kukamilika kwa miradi ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi I megawati 150 na Kinyerezi II megawati 240. Ujenzi wa miradi ulikamilika kwa asilimia 100 mwaka 2016 na mwaka 2018 mtawalia, ambapo jumla ya megawati 398.22 zimeingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

Aidha, ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) megawati 2,115 unaendelea ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 85 kulingana na Mpango Kazi wa kazi zilizopangwa.

Vilevile, Wizara ya Nishati ambayo ndiyo msimamizi wa sekta husika, inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Rusumo megawati 80 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 61.

Jingine la kujivunia

INATOKA

30

ni uunganishaji Mikoa ya Lindi, Mtwara, Njombe na Ruvuma katika Gridi ya Taifa ambako kumewezesha kusitisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia mitambo ya mafuta mazito ambayo ilikuwa inaigharimu TANESCO wastani wa shilingi bilioni 15.3 kwa mwaka.

Katika kipindi hiki cha miaka mitano, Mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Makambako hadi Songea umekamilika tangu Septemba, 2018 na kuwezesha vijiji vyote 122 kuunganishiwa umeme.

Wizara imeendelea kusimamia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kilovoti 220 kwa ajili ya Mradi wa Treni ya Mwendu Kasi (SGR) awamu ya kwanza (Lot I) yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Dar es Salaam hadi Kingolwira, Morogoro.

Pia, utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini unaendelea ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya vijiji 9,112 vimeunganishiwa umeme ikilinganishwa na vijiji 2,018 vilivyokuwa vimeunganishwa umeme mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 351.54.

Mafanikio mengine ni kuendelea kutokuwa

# MIAKA MITANO YA MAFANIKIO SEKTA YA NISHATI



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akiwa pamoja na Balozi wa Sweden hapa nchini Anders Sjoberg wakiminya kitufe kwa pamoja kuashiria uzinduzi wa mradi wa Ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme KV 220 kutoka Makambako hadi Songea pamoja na vituo vya kupooza umeme KV 220/33 katika sherehe zilizofanyika Songea mkoani Ruvuma, Aprili 6, 2019.

na mgawo wa umeme nchini na kuwa na ziada ya umeme wa wastani wa megawati 325 kwa siku.

Halikadhalika, Wizara ya Nishati kupitia TANESCO imeendelea kusimamia na kuwezesha uzalishaji wa vifaa vya

kujenga miradi ya umeme nchini na hivyo kusitisha uingizaji wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo, mashineumba, nyaya na mita za LUKU ndani ya nchi na hivyo kurahisisha upatikanaji wa vifaa

hivyo. Uzalishaji huo pia umechangia ongezeko la ajira nchini.

Katika kipindi hiki, wateja wapya 1,293,528

INAENDELEA UK.

32



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kulia), akifurahi pamoja na wananchi wa Kijiji cha Kolo wilayani Kondo, baada ya kuwasha rasmi umeme katika Zahanati ya Kijiji hicho, Juni 20, 2019.



Mitambo ya umeme ya Kinyerezi II, inayozalisha umeme wa megawati 240.

# MIKA MITANO YA MAFANIKIO SEKTA YA NISHATI



Mwonekano wa ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika mradi wa Umeme wa Rusumo.

**INATOKA 31**

wameunganishiwa umeme na kufanya jumla ya wateja waliunganishiwa umeme hadi mwezi Aprili, 2020 kufikia 2,766,745 ikilinganishwa na wateja 1,473,217 waliokuwepo hadi Juni, 2015 sawa na ongezeko la asilimia 88.

Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa umeme (Overall Electricity Access rate) nchini kutoka asilimia 67.8 mwaka 2016 na kufikia asilimia 84.6 mwaka 2020.

Aidha, Serikali kupitia TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imeendelea kuunganisha umeme kwa shilingi 27,000 katika maeneo yote ya vijijini kulingana na Mpango wa Kupeleka

## Umeme Vijijini.

Mafuta na Gesi katika kipindi cha miaka mitano cha Serikali ya Awamu ya Tano, utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika sekta ndogo ya mafuta na gesi umepata mafanikio makubwa.

Kati ya mafanikio hayo ni kuongezeka kwa gesi asilia iliyogunduliwa kutoka futi za ujazo trilioni 55.27 mwaka 2015 na kufikia futi za ujazo trilioni 57.54 mwaka 2020 sawa na ongezeko la futi za ujazo trilioni 2.27.

Mafanikio mengine ni kuanza kwa shughuli za utafutaji wa mafuta katika Kitalu cha Eyasi Wembere ambapo visima vifupi viwili (2) vyenye kina cha urefu wa mita 300 vimechorongwa katika Wilaya ya Igunga Mkoa wa

Tabora na Meatu mkoani Shinyanga.

Pia, kumekuwa na ongezeko la kasi ya usambazaji wa gesi asilia ambapo katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Mtwara, jumla ya nyumba za wateja wa awali zaidi ya 1,000 zimefikishiwa miundombinu ya usambazaji gesi

asilia na viwanda 48 vimeunganishwa kufikia mwezi Aprili, 2020. Aidha, zaidi ya magari 400 yamefungwa mifumo ya matumizi ya gesi asilia ikilinganishwa na magari 60 yaliyokuwa yameunganishwa mwaka 2015.

Vilevile, uzalishaji wa gesi asilia umeongezeka kutoka wastani wa futi za ujazo bilioni 37 kwa mwaka 2015 hadi futi za ujazo bilioni 46 katika mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 24.

Kuongezeka kwa mchango wa gesi asilia katika kuzalisha umeme nchini kutoka asilimia 36 mwaka 2015 hadi asilimia 57 mwezi Aprili, 2020 ni mafanikio mengine katika sekta hii.

Siyo hayo tu, bali pia kumekuwa na ongezeko la ushiriki wa Watanzania katika miradi ya mafuta na gesi asilia ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2020 kampuni 457 zimeorodheshwa katika kanzidata iliyowezesha kampuni hizo kushiriki katika miradi mbalimbali.

Aidha, Bandari za Tanga na Mtwara zimehuishwa katika kupokea Mafuta ambapo Bandari hizo zimeanza kupokea Mafuta kuanzia mwezi Julai, 2015 na Julai, 2018 mtawalia.

Watanzania wanapaswa kujivunia pia

**INAENDELEA UK. 33**



Mitambo ya kupokelea Gesi asilia katika eneo la Kinyerezi jijini Dar es Salaam.



INATOKA

32

kuendelea kuimarika kwa Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Bulk Procurement System - BPS) ambao umeongeza uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini na kupunguza gharama za uagizaji.

Kupitia usimamizi wa Wizara ya Nishati, sekta hii pia imejenga uwezo kwa kudhamini mafunzo ya ufundi stadi kupitia vyyo vya ufundi stadi (VETA). Serikali imeendelea kutoa kozi mbalimbali zinazohusiana na mafuta na gesi katika vyyo vikuu hapa nchini kwa viwango vya Stashahada (Diploma), Shahada (Bachelor) na Uzamili (Masters)

Aidha, jambo jingine la kujivunia ni kupungua kwa uchafuzi (uchakachuaiji) wa mafuta kutoka wastani wa asilimia 19.2 mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa asilimia 4 mwezi Machi, 2020.

Bila shaka utakubaliana nami kuwa kufanyika kwa mambo hayo yote, maana yake ni kwamba matokeo mazuri yameonekana kutoka kwayo, na kwakuwa malengo yaliyowekwa yamefikwa, basi Watanzania wana kila sababu ya kujivunia mafanikio hayo.

# MIAKA MITANO YA MAFANIKIO SEKTA YA NISHATI



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akikagua migahawa iliyounganishiwa gesi asilia iliyoopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na baadhi ya nyumba zilizounganishiwa nishati hiyo katika eneo la Mwenge Mlakuwa, Februari 1, 2020.

Utendaji kazi wa aina hii unaleta matumaini makubwa kuwa huko tuelekeako, mambo yataendelea kuwa mazuri

zaidi. Hata hivyo, hilo litawezekana tu ikiwa tutaendelea kuwa na uongozi mahiri kama huu. Uongozi unaojali maslahi

ya Watanzania na Taifa kwa ujumla, na hivyo kujitoa kuwatumikia wananchi kikamilifu.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa matumizi ya gesi asilia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Februari 1, 2020.



Kazi ya ujenzi katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha megawati 2115 ikiendelea.



Kamishna wa Petroli na Gesi wa Wizara ya Nishati, Adam Zuberi (kulia), akikagua njia ya kisasa ya kubaini hitilafu ya moto katika hatua za awali katika chumba cha kuendesha mitambo kwa njia ya kisasa, katika moja ya kampuni za gesi, alipofanya ziara pamoja na Ujumbe wake, kuanzia Mei, 26 hadi Juni 3, 2020 kukagua usalama wa maghala ya kuhifadhi na kupakua mafuta pindi majanga ya moto yanapotokea.




Kamishna wa Petroli na Gesi wa Wizara ya Nishati, Adam Zuberi (wa pili kulia) na Ujumbe wake wakiwa katika ziara kukagua usalama wa maghala ya kuhifadhi na kupakua mafuta pindi majanga ya moto yanapotokea. Ziara hiyo ilifanyika kuanzia Mei, 26 hadi Juni 3, 2020 jijini Dar es Salaam.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (katikati) akiwasili katika Kiwanda cha kutengeneza Marumaru cha Goodwill kilichopo wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, kinachotumia gesi asilia katika shughuli za uzalishaji. Katibu Mkuu alikuwa katika ziara kutembelea mradi wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Mei 30 - Juni 1, 2020.

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



**Fika Ofisi ya Mawasiliano,**  
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma au  
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018  
**Nukushi** +255-26-2320148

 [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)